

Simbachawene azindua mifumo kuharakisha kesi za jinai

NA SAIDA ISSA, DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi na utawala Bora, Boniface Simbachawene, uzinduzi wa mifumo utaharakisha kesi za jinai kutolewa uamuzi kwa kasi jambo ambalo litakalowapatia wananchi haki zao kwa haraka.

Waziri huyo alieleza hayo kwenye hafla ya uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi (CMIS) na tovuti Kwa Ofisi ya Taifa ya mashtaka(NPS) katika Ofisi ya NPS, hafla iliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema kuwa mfumo huo ni muhimu katika kipindi hiki ambacho muelekeo wa Dk. Samia ni kuhakikisha utendaji wa majukumu mbalimbali unaafanyika kwa njia za kidijitali.

Alisema kuwa kupitia mifumo hiyo itakwenda kupunguza mafaili na ukibaki na faili unauliza kwanini umebakili nalo kwa siku zote, jambo ambalo litazidisha uwajibikaji na kuharakishwa wananchi kupata haki bila ya kuchelewa kutokana na urasimu wa watendaji.

Alisema kuwa mfumo huo utakuwa muarobalini wa kuhakikisha kwamba kesi na haki kwa watanzania zitakuwa hazichelewi na lengo kuu la mifumo ni kurahisisha utendaji kazi Kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kushughulikia kesi mbalimbali.

Kwa upande naibu waziri Katiba na Sheria, Pauline Gekul, alisema wizara hiyo inaendelea kutekeleza maagizo ya utoaji haki na itaendelea

kushirikia na taasisi ya eGA kuhakkisha haki inatendeka kwa wakati huku akiiomba serikali kusaidia kuongeza watumishi ambazo wanahitajika.

Naye katibu mkuu wizara ya katiba na sheria, Mary Matondo, alisema wizara hiyo imeendelea kupokea fedha kwa ajili ya kuboredha uwekezaji wa mifumo katika kuleta ufanisi wa utendaji kazi katika sekta na kuwapatia wananchi haki wanayostahili

Naye mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu, alisema kuwa mfumo huo ni nyenzo muhimu na utarahisisha kutunza kumbukumbu zote za majalada na kuanza kwa mfumo huo kutakua na taarifa zilizo sahihi na umeshaanza kutumiwa kwa majaribio na kuona umuhimu wake.

Alieleza kuwa kuna changamoto ya uchache wa watumishi, ufinyu wa bajeti na uchache wa vifaa hali ambayo imewafanya kutofungua mfumo huu katika wilaya mpya ambazo wameshatfungua ofisi 37

Huku Mkurugenzi wa mamlaka ya serikali mtandao Ega, Benedict Ndomba alisema lengo la mfumo huo ni kukusanya,kuchakata na kutunza taarifa za kesi Jinai.

Alisema kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao, imejipanga kufanya mageuzi katika utoaji wa huduma mtandao, sanjari na hilo tumejipanga kutekeleza kikamilifu matakwa ya kisheria, pamoja na maelekezo ya Rais ya kuhakikisha mifumo ya TEHAMA inawasiliana na kubadilishana taarifa.